TANGAZO LA SERIKALI Na. 864 la tarehe. 18/10/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)
556 11 october

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA-MIKINDANI YA MWAKA 2024

Jina
TS. Na. 217 la 2024

**1**. Sheria Ndogo hiii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani ya Mwaka 2024, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani ya Mwaka 2024 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama “Sheria Ndogo kuu”.

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

**2**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika Jedwali la Kwanza-

(a) katika Sehemu ya II, kwa kufuta kipengele cha 11;

(b) katika Sehemu ya VII, kwa kuongeza maneno “kwa Mwaka” mara baada ya neno “Ada” lililopo katika safu ya tatu ya mstari wa kwanza;

(c) katika Sehemu ya IX, kwa kuongeza mara baada ya kipengele cha 3, kipengele kifuatacho:

| | |
|---|---|
| 4. Wanyama wengine ambao hawakutajwa | 1,000.00 kila mmoja |

(a) katika Sehemu ya X, kwa-

(i) kufuta kipengele cha 8; na

(ii) kubadili mpangilio wa vipengele vya 9, 10 na 11 kuwa vipengele vya 8, 9 na 10;

(b) katika Sehemu ya XI, kwa-

(i) kuongeza maneno "wa Halmashauri" mara baada ya neno "sherehe" lililopo katika vipengele vya 13 na 14; na

(ii) kuongeza maneno "wa Halmashauri" mara baada ya neno "michezo" lililopo katika kipengele cha 15;

(c) kwa kuongeza mara baada ya Sehemu ya XIV maneno yafuatayo:

"Tanbihi: Malipo ya ada zilizoainishwa katika kipengele cha 1 hadi 31 yatalipwa kwa mwaka."; na

(d) kwa kuongeza mara baada ya Sehemu ya XVII maneno yafuatayo:

"Tanbihi: Malipo ya ada zilizoainishwa katika vipengele vya 1, 2, 3, 5 na 6 yatalipwa kwa mwaka.".

Dodoma,
29 Agosti, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi -OR-Tamisemi*